

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**WIZARA YA MAJI**

Simu: +255 (0) 26 2322602  
Tovuti: [www.maji.go.tz](http://www.maji.go.tz)  
Barua pepe: [ps@maji.go.tz](mailto:ps@maji.go.tz)



NBC Tawi la Mazengo,  
Barabara ya Kuu,  
S. L. P. 456,  
**40473 Dodoma.**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Waziri wa Maji Mhe. Prof Makame Mbarawa (Mb) ametengua uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mjini Mtwara (MTUWASA) Mhandisi Mashaka Sitta kuanzia tarehe 8 Aprili, 2019 na anatakiwa kuripoti Wizara ya Maji ili kupangiwa majukumu mengine.

Katika hatua nyingine, Katibu Mkuu Wizara ya Maji Prof. Kitila Mkumbo kwa kushauriana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, amemsimamisha kazi Katibu Tawala Msaidizi (Maji), mkoa wa Ruvuma Mhandisi Genes Kimoro ili kupisha uchunguzi wa tuhuma zinazomkabili, ikiwamo kutekeleza miradi ya maji chini ya kiwango.

Kufuatia hatua hiyo, Katibu Mkuu Wizara ya Maji Prof. Kitila Mkumbo ameunda timu ya watalaam kuchunguza suala hilo mara moja.

**Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano**  
09.04.2019